# SEHEMU YA KWANZA

Mwanangu vyumba vimeisha na usiku huu kwa bei uliyonayo huwezi pata chumba zaidi nikusihi uondoke hapa, na usiku huu eneo hili ni baya sana kwa mtoto wa kike kama wewe, hata kama utapata chumba bado sikushauri kwani vyumba vingi ni vya biashara za wanaojiuza. Vyumba vya eneo hili havitaki wanaolala, hapa ni show time masaa matatu kwa manne.

Na unavyoonekana bado mdogo sana kiasi kwamba naogopa hata kukupokea lakini kwa kuwa mabinti wa siku hizi mna tamaa za maisha na kukimbilia Dar mkifikiri ni rahisi kutoka kimaisha kunawaponza na kuwafikisha hapa.....

(Mananeo yaliendelea kumtoka Mama aliyekua akisimamia nyumba ya wageni baada ya kuingiwa huruma kwa kumuona binti mdogo akiwa kavaa vizuri kwa kujisitiri usiku wa saa tano akitafuta chumba uchochoroni na sehemu yenye mengi kama ile).

Binti umefikia wapi?  umetoroka? ni mgeni wa hizi shughuli? Aliuliza mama yule huku huruma ikimjia kwa jinsi binti yule alivyoonekana. Binti aliendelea kukaa kimya akiwa mwenye mawazo.

Unaitwa nani, usiniletee uchuro mapema hii, umegeuka bubu ghafla, nitolee shida zako........ (kabla hajamaliza binti aliomba msamaha) Samahani mama yangu najua upo eneo la biashara bahati mbaya rafiki yangu alinielekeza kumbe sikuelewa, nilihitaji sehemu ya kujisitiri siku moja ili ratiba zangu ziendelee kesho, maelezo niliyopewa nimechanganya hata kufika hapa.

Nilielekezwa kinondoni ingekua rahisi kwangu kwa ratiba ya kesho, kutoshika maelezo kumenifikisha hapa, samahani mama.

Mama alijibu "Vyumba vimejaa na mazingira mazima nimekueleza jaribu kutafuta ustaarabu mwingine na mimi siwezi kukupokea hapa ikiwa sikufahamu na sijui umetoka wapi, isije kuniletea shida hapa na pia una pesa ndogo sana kiasi ambacho siwezi kuua chumba kimoja ambacho kingenipa mara nne ya pesa yako"

Sawa asante, binti alitamka maneno na kisha kutoka eneo lile la mapokezi kwa kuutafuta mlango wa kutokea.

Mtaa huo ulitawaliwa na bar na vijiwe vya pombe, mzunguko wa watu ulikua mkubwa hasa wanawake waliovalia mavazi ya usiku, kwa maneno aliyoambiwa na yule mama wa mapokezi alikumbuka na kujionea akiwa anapita kuelekea nyumba ile ya kupumzika, kuna baadhi ya wanaume walimsumbua bila staha na maneno yao huku wengine wakitaka kujaribu kumshika n.k

Kiukweli ilikua mara yake ya kwanza kushuhudia usiku unavyokua hasa kwa wanawake wanaojiuza na wanaume wanaonunua wanawake, alishangaa sana nyumba zile za kupumzika kuwa na aina ile ya biashara kwamba watu wanalipa kwa muda mchache. Kinyaa kilimuingia ghafla akawaza kwenda kulala kituo cha mabasi huku hofu yake ikiwa wapi atapata usafiri utakao mfikisha angalau ubungo kuliko eneo lile.

Akiwa katoka ile nyumba ya mapumziko, yule mama huruma na wasi wasi viliendelea kumjaa kwani alikumbuka mbali. Alikumbuka ndoto zake na malengo yake kama akibahatika kupata mtoto wa kike toka akiwa kijana hata alipofika utu uzima na kuingia kwenye ndoa (Mama yule alibahatika kupata watoto wawili wote wakiwa wa kiume na sasa wanajitegemea). Picha zilimjia na kwa jinsi muonekano wa yule binti alivyojisitiri akiwa mwenye afya ndoto na tamaa zilirudi upya.

Kwa muda mfupi alifikiria mengi sana maisha ya mabinti wa pale kwenye biashara yake ya nyumba ya wageni na kuona kwamba hata waliofika pale ni kwa sababu ya kukosa msaada na muongozo, kwa ujumla akafikiria kwa muonekano wa yule binti sidhani kama anajihusisha na hii michezo au biashara ya mazingira yale na hata kama anajihusisha ni mgeni.

Masai natoka hapa dakika tano naomba niangalizie, kama kuna chumba kitarudishwa wataweka saini hapa na funguo baki nazo na kama mtu atahitaji chumba unaweza muonesha, vyumba vilivyo wazi ni vitatu vya upande ule bei za show time unazijua na muda ni masaa matatu matatu. Vyumba vile viwili ni vya wanawake wale wanaovilipia hivyo haviingiliani, wakija na wateja wao waingie tu wape funguo....... (Mama yule aliendelea kuacha maagizo kwa muangalizi wa eneo lile kisha akatoka).

Alizunguka eneo lile zaidi ya dakika kumi bila mafanikio ya kumuona yule binti. Mungu wangu yule mtoto sijui kaelekea wapi, dakika chache hizi haonekani au kaanguka sehemu, kashawishiwa au asijekua kabakwa?! Mama yule aliendelea kujiuliza maswali mengi sana na wasi wasi uliendelea kumuingia akijiona mwenye hatia kwani lile eneo lilikua hatari sana kwa mtu aliyeonekana mgeni iwe jinsia yoyote ile alisumbuliwa sana na wanaume na wanawake wafanya shughuli zile kwa kufikiriwa ni waandishi wa habari wanaokuja kurekodi na kuwapiga picha.

Aliwaza hivyo na hofu juu huku akielekea eneo la bara bara kuu zilipo stand, upande wa pili alimuona binti kakaa kwa mama ntilie akavuka haraka kumfuata.

Mwanangu kumbe bado hujala?Aliuliza yule mama.

Heka heka za leo mama, niliwaza nipate sehemu ya uhakika ndipo nirudi kupata chochote kabla sijapumzika kwa ajili ya kesho. (Binti alijibu akishangaa kumuona yule mama pale)

Mpe chai kwanza akisubiri chakula na mimi nipatie chai pekee, usijali mwanangu kula nitalipa kisha naomba turudi wote, utalala ninapolala mimi ili asubuhi uamkie kwenye shughuli zako, usiku huu eneo hili si zuri kwa binti mdogo kama wewe mbali na michezo ya hapa polisi wapo nje nje unaweza kamatwa ukawekwa ndani.

(Mama alisisitiza akimsubiri binti apate chakula kisha warudi wote apate kumsitiri).

Baada ya kumaliza kula alimuuliza mizigo yake aliyokua nayo lakini hakua nayo zaidi ya begi dogo la mkononi ambalo lilikua na mtandio, nguo za ndani, nguo ya juu, mafuta, marashi na kioo.

Walirejea pamoja hadi kwenye nyumba ya mapumziko, karibu sana na leo utapumzika hapa bure sitakulipisha kitu jisikie huru, utalala ninapo lala mimi... Naitwa Mama Rahim ni mwenyeji wa Singida nina watoto wawili wote wa kiume wa mwisho anaweza kua kakuzidi kidogo anaitwa Shabani yupo Morogoro, haja bahatika kuwa na familia wala mtoto kama kaka yake ambaye ana mtoto na mwanae nipo nae kwangu, kabla sijaendelea kwa uchache wa utambulisho wangu naomba nikutambue pia kwa majina yako unakotoka na kuendelea.

Nashukuru kwa kunikaribisha eneo lako, nisamehe kwa awali kama nilikukosea kwa ukimya wangu hata ukakasirika, naitwa Siah John asili yetu ni kilimanjaro ila nimezaliwa na kukulia Tabora baba alikua akifanya kazi kule katika bodi ya tumbaku na hata shule nimesomea huko nikaja Dodoma kisha Morogoro chuo....(kabla hajamaliza Mama Rahim alimkatisha)

Hilo jina kidogo liwe kama lile nilihitaji kumpa mwanangu kama ningebahatika kupata mtoto wa kike, limepishana kidogo sana. Nilipanga nitampa jina Sierra ambalo lilikua jina la rafiki yangu wa kizungu, yule dada alikua mpole mwenye huruma nilimpenda kwa kila kitu na jina lake nilitamani nimpe mwanangu kama ukumbusho na nilitamani awe kama yeye (alivuta pumzi kidogo kisha aliendelea). Mungu huyu, vipi kama ningekuacha damu ingenililia hata majina unaelekea na mwanangu, nakuona kama mwanangu Siah.

Umetokea wapi usiku huu mwanangu? Kuna shida sehemu? Umefukuzwa? Unaelekea wapi? Maana hauna hata mizigo…….. Kiukweli hamna shida yoyote Mama Rahim zaidi nilifikiri ningefanikiwa mapema ila sikufanikiwa na maelekezo niliyopewa nimechanganya hata kufikia hatua hii ila Mungu akipenda Kesho nitafanikiwa najua. Siah alijibu japo sauti na uso wake ulionesha tofauti na alichoongea.

Mama Rahim aliuliza maswali aliyouliza awali akihitaji sana ufafanuzi akakumbuka kwa mtu aliyekumbwa na majanga ni ngumu sana kuongea, akaendelea. Utalala hapa leo naomba unisubiri kidogo nikakuoneshe sehemu tutakayolala kisha asubuhi na mapema tutaenda kwangu ukapaone ili hata ukikwama utarudi na mimi nitakuwepo nyumbani kwangu Kesho, hapa nimekuja kushika mara moja kijana anaekuepo hapa hayupo kwa leo.

Sawa Mama, nashukuru sana kwa kunikaribisha na kuniruhusu nilale hapa leo. Ukimya ulipita kidogo huku Siah akiendelea kusubiri kuonyeshwa sehemu atakayo lala, alijionea mengi eneo lile yanayofanyika usiku ule biashara ya ngono wazi wazi na namna madada wanavyojiachia na mavazi yao yasiyositiri miili yao. Baadaye alionyeshwa akapumzika japo alipumzika peke yake mpaka saa kumi na moja asubuhi alipokuja Mama Rahim kumuamsha waondoke kuelekea kwake.
“Twende mwanangu kumekucha tayari, tutamalizia usingizi nyumbani sehemu nzuri zaidi na pia usafi tutafanya huko pamoja na chai na mambo mengine” Mama Rahim alimuamsha Siah na kuondoka nae kuelekea kwake kupisha wapika supu kwenye nyumba ile pia wafanya usafi wa eneo lile kuendelea na shughuli zao wakati yeye anaenda……………..